## Maswali

1. Paulo alikuwa anaenda nini Rumi?
2. Mbona nahodha hakutaka kukaa kwa Bandari Nzuri?
3. Paulo aliwahadharisha eti nini?
4. Nini ilifanyika walipotaka kwenda kwa bandari kubwa?
5. Paulo alihimiza kila mtu eti nini?
6. Nini ilifanyika kwa meli walipokuwa wanakaribia pwani?
7. Kila mtu alifika nchi kavu namna gani? Kila mtu alipona?
8. Jina la kisiwa walichoenda kiliitwa nani?
9. Nini ilifanyika kwa Paulo walipokuwa wakiasha moto? Aliumia?
10. Paulo alisaidia watu wa Malita namna gani?

## Majibu

1. Paulo alikuwa anaenda Rumi kuhukumiwa na Kaisari.
2. Hiyo bandari ilikuwa ndogo. Hakutaka kukaa kule wakati wote wa kipupwe.
3. Paulo aliwahadharisha kwamba wasisafiri kabla ya kipupwe kuisha.
4. Kulikuwa na dhoruba ya ajabu iliyovuma hata wakapotezwa.
5. Paulo alisema kwamba malaika alimwambia asiogope, wote wataokoka.
6. Meli iligonga ukingo mgumu.
7. Baadhi ya watu waliogelea, wengine walielea kwa vipande vya mbao. Wote waliokoka.
8. Kisiwa kiliitwa Malita.
9. Paulo aliumwa na nyoka wa sumu. Hakuumia.
10. Paulo aliponya watu wengi kwa kisiwa cha Malita.

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2    Mwaka wa 2

# 101 Meli ya Paulo inavunjika

### Kwa Biblia

Matendo ya Mitume 27:1—44


### Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Paulo alikuwa na imani kwa Mungu hata wakati wa dhoruba kuu. Mungu alilinda na kuokoa Paulo kutoka kwa dhoruba

### Somo

Paulo alianza safari yake ya kuenda Rumi. Alikuwa anaenda kuhukumiwa huko Rumi na Kaisari. Paulo alikuwa mmoja wa wafungwa wenye walikuwa wanapelekwa na akida,jina lake Yulio. Walisafiri kwa meli yenye ilikuwa inaenda Rumi ikipeleka misiko ya ngano.


Upepo ulitusumbua na ukafanya safari ikawa polepole sana. Meli ilisimama kwa bandari iliyoitwa Bandari Nzuri kwa kisiwa cha Krete. Tayari ilikuwa wakati wa masika. Ilikuwa ni hatari meli kusafiri wakati wa mwisho wa masika au wakati wa kipupwe (baridi) kwa sababu kulikuwa na dhoruba kubwa. Paulo alikataza nahodha wa meli na Yulio kwamba wasiendelee na safari mpaka mwisho wa hayo majira.



Bandari nzuri ilikuwa ndogo sana. Nahodha hakutaka kuishi hapo wakati wote wa kipupwe. Aliamua kwenda kwa bandari kubwa kule krete.

Waliongoja upepo wa kusini uvume na bahari itulie, halafu wakaanza safari. Kwa ghafula upepo ulibadilika na dhoruba ikavuma. Upepo ukawa wa nguvu. Meli haingeenda wakati wa upepo mkali. Waliachilia upepo upeleke meli popote.

Meli ilisukumwa ikaelekea upande mwingine na wakapotea walikokuwa wakienda. Meli ilianza kuvunjika kwa ajili ya dhoruba kubwa. Mabaharia walifunga kamba kuzungusha meli chini ya matanga ili isiharibike zaidi. Nahodha aliogopa akiona kwamba watasukumwa kwa mchanga nyingi iliyoko kwa pwani ya kaskazini ya Afrika. Mabaharia walitelemsha tanga ili wazukumwe polepole.



Upepo uliendelea kuvuma. Uliendelea kuwa wa nguvu. Meli iliyumbishwa yumbiswa. Mabaharia walitupa mizigo baharini ili meli iwe nyepesi. Siku iliyofuata tena wakatupa vyombo vyao. Lakini upepo uliendelea kuwa mwingi. Hawakujua wako wapi. Hawakujua wako wanaelekea upande gani. Walipotelea katikati ya bahari kabiza.

Kila mtu hakukuwa na tumaini la kufika nchi kavu. Kwa siku nyingi hakuna aliyekula chakula. Lakini Paulo alikuwa na ujasiri. Aliamini Mungu. Aliwambia, “Msiogope. Jana usiku, malaika wa Mungu aliniambia nisiogope. Sisi wote tutafika kwa nchi kavu salama. Hakuna atakayezama. Lakini meli itavunjika yote.”

Baadaye, usiku moja, mabaharia walikundua kwamba wako karibu na ukingo wa bahari. Walitupa nanga ili meli ishikwe vizuri. Kila mtu aliongoja kuche siku ingine ili waone nchi kavu tena. Paulo aliwahimiza wakule chakula.

Baadhi ya mabaharia walitaka kujiponya pekee yao. Walikuwa wanatorokea kwa mashua ndogo. Walijifanya kama wanaendelea kutupa nanga zingine. Paulo aliwaona wakitaka kutoroka. Aliambia akida, “Ikiwa hawa watu watatoroka, hamtapona wote.” Walitakiwa watu wa kusukuma meli mpaka ukingo wa bahari.

Akida aliambia watu wakate kamba za mashua ndogo. Mashua ilianguka baharini na ikachukuliwa mbali.

Kulipobambazuka mabaharia waliona ukingo wa bahari. Lakini hawakujua nchi hiyo. Waliona kwamba hiyo pwani yote ilikuwa na miamba. Kulikuwa na ufuko na wakafikiria watasukuma meli kule. Mabaharia walivuta nanga na kuendesha meli. Meli iliendelea kuenda ukingoni.

Ghafula, kukawa na mshindo mkuu. Meli iligonga kwa ukingo mgumu. Mabaharia hawakuweza kusongesha meli karibu na pwani tena. Meli ilivunjikia kwa ukingo mgumu. Mawimbi mazito yalianza kuvunja meli.

Askari walitaka kuua mahabusi wote ili wasitoroke. Lakini akida alitaka kuokoa Paulo. Aliamrisha mahabusi waruke ndani ya maji na waogelee waende kando. Waliojua kuogelea waliruka kwa maji na kuogelea. Waliogelea mpaka kando. Wengine walivuka kwa kuelea wakitumia vipande vya mbao vilivyo vunjika kutoka kwa meli. Kila mtu aliyekuwa melini alifika kwa nchi kavu salama.



Walikuwa wametua kwa kisiwa kilichoitwa Malita. Watu wa Malita walikuja kusaidia kila mtu aliyetoka kwa meli iliyovunjika. Walitengeneza moto mkubwa kwa sababu kila mtu alikuwa na baridi. Ilikuwa inanyesha na kulikuwa na baridi nyingi.

Paulo alisaidia kuokota guni ya kuweka kwa moto. Alipokuwa akitupa guni ndani ya moto, nyoka wa sumu alikuja na akamuuma mkono. Lakini Mungu alikuwa analinda Paulo, na hakuumia kutokana na kuumwa kwa nyoka.

Paulo na wote waliotoka kwa meli walikaa kwa kile kisiwa kwa miezi mitatu mpaka walipoona ni salama kusafiri tena. Paulo aliponya wagonjwa wengi kwa kisiwa cha Malita. Aliponya baba wa aliyekuwa kiongozi wa kisiwa. Watu wa Malita walikuwa wazuri kwao. Baadaye waliwapa chakula walipokuwa wakiendelea na safari ya kuenda Rumi.